TUKI
KAMUSI YA KISWAHILI-KIINGEREZA
Swahili-English Dictionary

TOLEO LA KWANZA

TAASISI YA UCHUNGUZI WA KISWAHILI
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM
2001

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S. L. P. 35110,
Dar es Salaam

© Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) 2001
Toleo la Kwanza 2001

ISBN 9976 911 44 0

Haki imehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigisha chapa au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

496.392
PL K919t
8763cop.2
.K93
2001
IAS Ref

DIBAJI YA TOLEO LA KWANZA LA KAMUSI YA KISWAHILI-KIINGEREZA

Kamusi hii ya Kiswahili-Kiingereza ina historia ndefu. Wazo la kutunga kamusi hii ilianzishwa mwaka 1964 na Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili (ambacho kuanzia mwaka 1972 kilijulikana kama Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili). Wazo hili lilibuniwa wakati wa enzi ya Profesa Wilfred H.Whitely, ambaye wakati huo alikuwa ndiye Mkurugenzi wa Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, ikiwa ni miaka 25 baada ya kuchapishwa kwa kamusi ya Johnson ijulikanayo kama *Standard Swahili-English Dictionary* (1939). Kazi ya utunzi wa kamusi mpya ilianza baada ya shirika lijulikanalo kama *Calouste Gulbenkian Foundation* kutoa msaada wa pesa kwa Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 1964 hadi Octoba 1967 ili kukiwezesha chuo kumwajiri mchunguzi atakayeweza kuifanya kazi hiyo.

Katika kutekeleza azma hiyo, Chuo kilimwazima Bwana J.A.Tejani kutoka Wizara ya Elimu Zanzibar na kumwajiri kama Mchunguzi. Bwana Tejani wakati huo alikuwa na shahada ya B.A. katika lugha za Kiarabu na Kiajemi ya Chuo Kikuu cha London, na alikuwa pia na ujuzi katika lugha za Kigujarati, Kiurdu na Kiswahili. Ilipangwa kuwa Mchunguzi Tejani angekuwa anasaidiwa na Mchunguzi Msaidizi na angeshauriwa na Miss M.A. Bryan wa *School of Oriental and African Studies* (SOAS), London Profesa E. Dammann wa Marbury na Profesa D.A. Olderogge wa Leningrad.

Bwana Tejani alipokuwa Mkurugenzi wa Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili kati ya mwaka 1968 na 1969, aliendelea kuifanya kazi hii hadi mwaka 1970 alipoikabidhi kwa Mkurugenzi mpya wa Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, Bwana George Mhina. Mwaka 1967, kabla ya kuteuliwa kwa Mkurugenzi mpya, Baraza la Kiswahili la Taifa lilikielekeza Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili kuwa kamusi inayopaswa kuandaliwa mwanzo iwe kamusi ya Kiswahili-Kiswahili na wala sio kamusi ya Kiswahili-Kiingereza. Kwa hiyo mwaka 1970 kazi ya kwanza ya Mkurugenzi mpya, Bwana George Mhina, ilikuwa ni kuhakikisha kuwa vitomeo vyote vilivyomo katika kamusi ya Kiswahili-Kiingereza iliyoanzishwa na Tejani vinatafsiriwa upya katika Kiswahili. Mswada wa kamusi ya Kiswahili-Kiswahili ulikamilika Juni 4, 1978 na kamusi ikatoka mwaka 1981.

Mwaka 1972, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ilimpata mtaalamu wa kamusi kutoka Poland, Profesa Rajmund Ohly. Kwa kuanzia profesa huyu alipewa kazi ya kutunga kamusi ya Kiingereza-Kiswahili. Hata hivyo, mwaka 1975, Taasisi ilipounda jopo la wataalamu wa kamusi ili kukamilisha kazi ya kutunga kamusi ya Kiswahili-Kiswahili, Profesa Ohly alisitisha kazi ya kutunga kamusi ya Kiingereza-Kiswahili na kujiunga na jopo la kamusi ya Kiswahili-Kiswahili.

aa pia **ahaa** *ki* (kutegemea kiimbo) ah!

aalam* *kv* (Mungu pekee) the most knowledgeable: *Allahu* ~ Almighty God, the most knowledgeable. (Kar)

aali* *kv* (vitu) superior, great; exalted: *Haya ni mambo* ~ these are great (exalted) things. (Kar)

aalimu* *nm* [*a-/wa-*] 1 educated man (in islamic knowledge). 2 scholar. *kv* having profound islamic knowledge. (Kar)

aathari* *nm* relic, ruins. (Kar)

abaa! *ki* hallo! hey!

abadani!* *ki* not at all, never: *Hutakubaliwa* ~ you will never be accepted. (Kar)

abadi* *kl* forever, eternity, always, permanently: *Tatizo hili sasa* ~ this is now a permanent problem. (Kar)

abakusi pia **abaki** *nm* [*i-/zi-*] abacus.

abedari* *nm* [*i-/zi-*] pulley used on dhows. (Kar)

abee! pia **bee**! *ki* (wanawake) word used in response to summons or address.

abir.i[1]* *kt* [*ele*] sail, navigate, travel. (*tde*) **abiria**, (*tden*) **abiriana**, (*tdew*) **abiriwa**; (*tdk*) **abirika**; (*tds*) **abirisha**. (Kar)

abir.i[2]* *kt* [*ele*] forecast; foretell; predict. (*tde*) **abiria**, (*tdn*) **abiriana**, (*tdew*) **abiriwa**; (*tdk*) **abirika**; (*tds*) **abirisha**. (Kar)

abir.i[3]* *kt* [*sie*] learn from experince or incidents. (*tde*) **abiria**; (*tdk*) **abirika**; (*tds*) **abirisha**. (Kar)

abiria* *nm* [*a-/wa-*] passenger: *Gari moshi la* ~ passenger train; *Gari la* ~ bus; *Mizigo ya* ~ passenger luggage. (Kar)

abjadi* *nm* [*i-/zi-*] alphabet: ~ *za Kiswahili* Swahili alphabet; ~ *za Kirumi* Roman alphabet. (Kar)

ablauti* *nm* [*i-/zi-*] ablaut. (Kng)

abra* *nm* [*i-/zi-*] chance, opportunity, spare time: *Sina* ~ I have no time; *Sijapata* ~ *ya kuongea nao* I haven't had an opportunity to talk to them. (Kar)

abtali* *nm* [*wa-*] heroes, heroin (us. of war). (Kar)

abu* *nm* [*a-/wa-*] father. (Kar)

abud.u[1]* *kt* [*ele*] 1 worship: ~ *Mungu mmoja* worship one God. 2 idolize. 3 adore, love: ~ *kazi* adore work; ~ *usingizi* adore sleep. (*tde*) **abudia**, (*tden*) **abudiana**, (*tdew*) **abudiwa**; (*tdk*) **abudika**; (*tds*) **abudisha**. (Kar)

abudu[2]* *nm* [*a-/wa-*] toy. (Kar)

abunusi* *nm* [*u-/i-*] ebony: *Samani za* ~ ebony furniture. (Kar)

abunuwasi* *nm* [*a-/wa-*] cunning character in Arabic tales. (Kar)

aburani *nm* [*i-/zi-*] pledge.

abuwabu* *nm* [*i-*] doors: ~ *iko wazi* the doors are open. (Kar)

abwe! pia **ebo**! *ki* wow!

abyadhi[1]* *kv* white: *Shati* ~ a white shirt. (Kar)

abyadhi[2]* *nm* [*i-*] playing card or dice which has no number on it. (Kar)

ach.a[1] *kt* 1 quit/stop doing sth, recant, desist: ~ *ulevi* quit/stop drinking; ~ *kazi* quit job; ~ *kukohoa* stop coughing. 2 leave behind: *Wasafiri wame*~ *mizigo yao nyuma* passengers left their luggage behind. 3 abandon, discontinue, neglect, chuck in, come away, discard, desert: *Watu wame*~ *mashamba yao* people have neglected their farms; *Kuku ame*~ *watoto wake* the hen has deserted her chicks; ~*na naye* leave him/her alone. 4 abdicate. 5 acquit, release, pardon: ~ *mfungwa huru* pardon a prisoner; ~ *mshtakiwa huru* acquit a defendant. 6 allow, let, permit, forgo, give leave: ~ *apite* allow him/her to pass; ~ *apumzike* let him/her rest. 7 separate from, divorce: *Amemw*~ *mkewe* he has divorced his wife. 8 leave sth somewhere: ~ *kitabu mezani* leave a book on a table; ~ *ujumbe ofisini kwangu* leave a message at my office; ~ *posta upande wa kushoto* leave the post office on your left hand side. 9 abjure. 10 break: ~ *tabia*